



NAFASI YA MAFUNZO YA UMEME NURU

Jumuiya ya Nishati Jadidifu Tanzania (Tanzania Renewable Energy Association–TAREA) imepokea usaidizi wa fedha kutoka Umoja wa Nchi za Ulaya na Serikali ya Ujerumani kupitia mpango wa Uwezeshaji Vijana Kupata Ujuzi na Ajira – Africa (Employment and Skills for Development in Africa-E4D) wa Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Ujerumani (Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit-GIZ), unao shirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu katika kuwajengea uwezo vijana kuweza kujajiri katika fani ya ufundi mchundo wa umeme nuru.

TAREA itaendesha mafunzo ya ufundi mchundo wa umeme nuru kwa kushirikiana na Chuo cha Ufundi-Arusha (Arusha Technical College).

Tunakaribisha maombi ya vijana kutoka mikoa ya Tanzania Bara isipokuwa Manyara na Simiyu ambayo vijana wake wamekwisha alikwa kwenye mafunzo.

Mradi utachangia gharama za: ukufunzi, kuishi wakati wa mafunzo Arusha, mazoezi katika kampuni na vifaa vya awali kuanzia kazi ya ufundi. Mshiriki wa mafunzo atatakiwa kuchangia nauli ya kufika Arusha na kurudi nyumbani.

Kijana anayetaka kujiunga na mafunzo haya anatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:

- 1) Awe kijana aliyehitimu kidato cha nne au darasa la saba aliyekwisha jihusisha na kazi za ufundi wa umeme wa majumbani, magari, simu au radio.
- 2) Kijana, mhitimu wa darasa la saba au kidato cha nne ambaye tayari anafanya kazi katika sekta ya umeme nuru, ufundi au mauzo, bila mafunzo rasmi.
- 3) Awe raia wa Tanzania na atatakiwa kuthibitisha wakati wa maombi kwa kuambatanisha nakala ya kati ya vifuatavyo:kadi/namba ya NIDA, pasi ya kusafiria, cheti cha kuzaliwa au barua ya mtendaji kijiji. Ikiwa ni barua ya mtendaji wa kijiji, barua iambatane na kivuli cha kadi ya NIDA/Namba ya NIDA ya mtendaji.
- 4) Awe kijana ambaye yuko tayari kupanda juu, kama paa au ngazi ndefu.
- 5) Taarifa muhimu ziwemo katika barua ya maombi: jina lako kamili, anwani yako, mahali unapotoka (kijiji/mji au halmashauri), namba ya simu/Whatsapp/barua pepe kwa mawasiliano ya haraka, na jina na namba ya simu ya mtu wa karibu.
- 6) Wasichana wanahamasishwa kuomba kwani watapewa kipaumbele katika mafunzo haya.

Maombi yawasilishwe kwa fomu iliyopo hapa chini, au uiombe kwa Whatsapp 0755 086 462. Uirudishe kwa njia ya barua pepe ikibeba kichwa cha habari **Maombi ya Mafunzo ya Umeme Nuru** kwenda anwani hii: matimbwi@tarea-tz.org au Whatsapp 0755 086462. Mwisho wa maombi ni **03/03/2023**. Barua iandikwe kwa Katibu Mtendaji, S.L.P 32643 Dar es Salaam

Matimbwi

Dr.-Ing. Matthew Matimbwi
Katibu Mtendaji-TAREA

Implemented in Tanzania by:



VET Toolbox partner:



P.O. Box 32643
16106 Dar es Salaam
Tanzania
Email: info@tarea-tz.org



Mobile: +255 755 086 462
Mobile: +255 714 560 566
Mobile: +255 713 934 527
Website: www.tarea-tz.org

Visiting Address: Mandela Road, Plot 1080 Mabibo External, Export Processing Zones, Shopping Arcade 17

MAOMBI YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI MCHUNDO WA UMEME NURU

Jina

Jinsia

Tarehe ya kuzaliwa

Kijiji

Halmashauri

Mkoa

Namba ya simu

Barua pepe

Anwani

Elimu yako

Umewahi kufanya kazi za ufundi? Kama ndiyo, eleza

Viambatanisho	Nakala za:
	1.0 Cheti cha shule
	2.0 Kadi ya NIDA au Kadi ya mpiga kura au barua ya mtendaji

Tuma fomu hii kwa barua pepe kwenda matimbwi@tarea-tz.org au Whatsapp 0755086462

Implemented in Tanzania by:



VET Toolbox partner:

